

Picha na Hoda Baraka, Survival Media Agency

# Tukisimama katika Mamlaka yetu:


## Madai ya Wanawake na Wasichana wa Kiafrika kwa ajili ya COP27

## UTANGULIZI

Mazungumzo kuhusu tabianchi mwaka 2022 (COP27) yatafanyika katika bara la Afrika kwa mara ya kwanza baada ya miaka sita. Katika muktadha huo, Wafeminia wa Kiafrika wamekusanyika kutoka kanda zote tano za bara hili ili kuzindua madai ya pamoja ambayo yanapaswa kushughulikiwa wakati wa mkutano wa COP27. Wafeminia wa Kiafrika waliochangia katika andiko hili la madai ya pamoja wanafanya kazi ndani ya mfumo wa ikolojia ya tabianchi ili kusukuma na kuongeza hatua katika mada mbalimbali za kipaumbele, ikiwa ni pamoja na uongozi wa wanawake na vijana katika michakato ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, mabadiliko ya nishati, fedha, teknolojia, na mahitaji yanayohusiana na haki katika masuala ya tabianchi, ya kijamii, na ya kiuchumi.

African Feminist Taskforce

WOMEN & GENDER CONSTITUENCY





*Picha ya kushoto Annabelle Avril, WECF*
*Picha ya kulia Hoda Baraka, Survival Media Agency*

# MUKTADHA

Ripoti ya hivi punde kutoka kwa Jopo la Serikali mbalimbali kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (IPCC) kwa mara nyingine tena inathibitisha usemi wa wafeminia kwamba mabadiliko ya tabianchi ni tishio na janga kubwa kwa ustawi wa jamii zetu na kwa afya ya ulimwengu.
Kwa mujibu wa tathmini ya sita ya IPCC (ya mwezi Februari 2022), mabadiliko ya tabianchi yanayochochewa na binadamu yanasababisha uharibifu hatari na mkubwa katika mazingira asilia na hivyo kuathiri maisha ya mabilioni ya watu duniani kote.[1] Mifumo ya ikolojia na watu wasio na uwezo wa kustahimili ndio wanaoathirika zaidi. Ingawa mabadiliko ya tabianchi yanaathiri maeneo yote yenye watu, nchi ambazo zinategemea zaidi maliasili kwa ajili ya maisha yao zimeathirika kwa namna kubwa zaidi. Wanawake kutoka katika nchi hizo kwa kawaida wanakabiliwa na hatari nyingi na kubeba mizigo mikubwa zaidi kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi, mfumo dume, umaskini uliokithiri, na kuongezeka kwa ukosefu wa usawa.

Afrika inaongezeka joto kwa kasi zaidi kuliko wastani wa kimataifa na ripoti ya IPCC inadhani kuna uwezekano mkubwa kwamba Afrika yote itaendelea kuwa na joto katika karne ya 21.[2] Tofauti kubwa zaidi ya mvua imesababisha ukame mkali zaidi na mafuriko, na kuongeza maeneo ambayo tayari yana maafa. Kutokana na ongezeko la joto, shida ya maji iliyopo itaongezeka, na hivyo kuweka shinikizo kubwa zaidi kwenye mfumo wa kilimo, hasa kwa wakulima wadogo na wazalishaji wa chakula—wengi wao wakiwa wanawake. Kwa jamii nyingi kote barani Afrika, mazingira asilia sio tu chanzo salama cha chakula, makazi, na nishati, bali pia chanzo cha urithi mkubwa wa tiba asilia, utamaduni, desturi, na mkusanyiko wa karne za historia na ujuzi asili. Kushindwa kushughulikia mabadiliko ya tabianchi kunaweza sio tu kusababisha uharibifu wa mifumo ya ikolojia, bali pia kuharibu moyo halisi wa bara la Afrika.

---

1. https://www.ipcc.ch/assessment-report/ar6/
2. https://www.un.org/africarenewal/magazine/december-2018-march-2019/global-warming-severe-consequences-africa

Umoja wa Mataifa unakadiria kuwa asilimia 80 ya wakimbizi wa tabianchi ni wanawake.[3] Kaskazini Mashariki mwa Nigeria, kwa mfano, shughuli mbalimbali za kibinadamu zimeongeza kasi ya athari za mabadiliko ya tabianchi, na kusababisha uhaba wa rasilimali kama vile maji, chakula na ardhi. Takwimu za Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM) (2021) zilionyesha kwamba wanawake ni asilimia 53 ya Wakimbizi wa Ndani katika eneo lililoathiriwa na migogoro Kaskazini Mashariki mwa Nigeria.[4] Hata hivyo, wanawake—hasa wanawake wa Kiafrika—mara nyingi sana wanafungiwa nje ya meza za kufanya maamuzi na maeneo ya madaraka ambapo sera na miradi ya mabadiliko ya tabia nchi zinaundwa na kutengenezwa.

Ukubwa wa muunganiko wa athari umeelezwa vyema katika Ripoti ya Sita ya Tathmini ya IPCC ("Athari, Marekebisho, na Uwezekano wa kuathiriwa[5] - sehemu ya pili), ambapo ukoloni umetambuliwa kama mojawapo ya vichochezi muhimu vya mabadiliko ya tabianchi. Uthibitisho kama huu unatoa imani kwa wito wa kuzingatia haki kwenye kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi hasa kwa maeneo ya Kusini mwa Ulimwengu na kwa ajili ya maendeleo yenye dhamira ya kuleta mifumo mipya inayoondoka kwenye ukandamizaji na unyonyaji wa watu na ekolojia asili, kuelekea kwenye uhifadhi wa pamoja na ustawi wa jamii endelevu. Ripoti ilieleza tena kwamba kushughulikia ukosefu wa usawa katika upatikanaji wa rasilimali, mali, huduma, na kushiriki katika kufanya maamuzi na uongozi, ni muhimu kwa ajili ya kufikia haki za kijinsia na za mabadiliko ya tabianchi. Ilieleza zaidi kwamba hatua za makusudi za kisera, miradi ya muda mrefu na uwekezaji kwa ajili ya

3 https://www.bbc.com/news/science-environment-43294221
4 https://reliefweb.int/report/nigeria/northeast-nigeria-displacement-report-36-may-2021
5 https://www.ipcc.ch/assessment-report/ar6/




Picha na Hoda Baraka, Survival Media Agency

kusaidia mabadiliko katika sheria, kanuni za kijamii, na tabia ni muhimu kwa kushughulikia mifumo kandamizi na kuunda mazingira wezeshi kwa makundi yaliyotengwa ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Licha ya kukabiliwa na changamoto nyingi na mifumo ya kutengwa, wanawake wa Kiafrika, wasichana, na wazawa, wanafanya kazi kubwa na ya kipekee kulinda mazingira asilia na kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Njia za kutatua matatizo ya mahali husika ambazo zimejaribwa na kuthibitishwa kuwa za haki na zenye kuleta mabadiliko zinaweza kuonekana katika bara zima—kuanzia miradi ya **nishati ya endelevu** katika maeneo ya vijijini Uganda kwa ajili ya kaya na vyama vya ushirika vya kilimo, hadi **kuwawezesha wanawake wa vijijini kupitia maendeleo jumuishi, yanayostahimili mabadiliko ya tabianchi** nchini Ethiopia, hadi vikundi vya wanawake vya ndani nchini Nigeria vinavyojihusisha na Mfuko wafedha za kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Njia hizi za kutatua matatizo na nyingine nyingi ambazo zinaendelea kuandikwa na **kundi la watu wenye maslahi na maoni yanayofanana kuhusu Wanawake na Jinsia**, ni ushuhuda wa uongozi wa thamani wa wanawake mbalimbali katika mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi. Kwa hivyo, kuwekeza katika uongozi wao sio tu ni jambo sahihi na la haki kufanya, bali pia mkakati wa kupunguza ukali wa kutegwa kwao.






*Picha za juu na kushoto na Hoda Baraka, Survival Media Agency*
*Picha ya kulia Annabelle Avril, WECF*



# MADAI

## **Uwakilishi, uongozi, na ushiriki:** Wafeminia wa Kiafrika wanataka wanawake na vijana wajumuishwe katika mchakato wa kitaifa na katika ngazi za kufanya maamuzi UNFCCC. Tunadai

1. Uwakilishi sawa na ushirikishwaji ulio na maana wa wanawake, wasichana, watu wenye ulemavu, wazawa, na vijana kwa ujumla wao katika michakato yote ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika ngazi ya kimataifa na kitaifa.

2. Maarifa na fursa za kukuza ujuzi kwa wanawake, wasichana, na vijana kuhusiana na mchakato ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kusaidia ushiriki wao kama wajumbe wa kitaifa na katika sera ya kimataifa.

3. Kuweka vipaumbele vya uwekezaji katika utekelezaji na ufuatiliaji wa mpango kazi wa kuimarisha usawa wa kijinsia (GAP) wa UNFCCC, ikiwa ni pamoja na kuwezesha maafisa wanaosimamia ujumuishwaji wa masuala ya jinsia kwenye malengo ya kitaifa ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Mapitio ya muda wa kati ya maendeleo ya utekelezaji wa shughuli zilizomo kwenye mpango kazi wa jinsia yanaendelea. Mafanikio kadhaa yamerekodiwa, lakini bado kuna kazi kubwa ya kufanywa. Kusaidia maafisa wanaosimamia ujumuishwaji wa masuala ya jinsia kwenye malengo ya kitaifa ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi kutoka maeneo ya Kusini mwa Ulimwengu ni lazima kiwe kipaumbele ili nia ya mpango kazi wa jinsia utimizwe kikamilifu na ujumuishaji wa masuala ya jinsia kuharakishwa katika michakato na miradi yote ya kitaifa ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

## **Mageuzi ya haki na usawa kutoka kwenye utegemezi ya Mafuta ya Kisukuku (gesi chafu).** Tunadai

4. Nchi zilizoendelea zinahitajika kusitisha mara moja uwekezaji mpya katika gesi chafu na nishati ya nyuklia, kwa ajili ya mabadiliko ya haraka kutoka kwenye uchumi unaotegemea gesi chafu kuelekea uchumi endelevu, wa haki, na wa kifeminia unaozingatia usawa wa jinsia katika matumizi ya nishati mbadala.

5. Nchi zilizoendelea, hasa Umoja wa Ulaya, zinawajibika kujiondoa kwenye mapatano ya mkataba wa nishati na kusitisha upanuzi wake katika nchi nyingine. Mkataba huo unaruhusu mashirika yaliyowekeza kwenye uzalishaji wa makaa ya mawe, mafuta na gesi chafu kuzuia mabadiliko ya mfumo wa nishati safi kwa kuyapa mashirika hayo mamlaka ya kuzishitaki serikali katika mahakama za siri na mbele ya wasuluhishi wa kibiashara ambao motisha wao si kulinda sayari, bali kulinda maslahi ya mashirika kama hayo.[6]

---

6 https://friendsoftheearth.eu/energy-charter-treaty/

6 Kuwa na mpango mahusisi wa kusaidia jamii zilizo maskini zaidi na zilizo hatarini zaidi za Kiafrika, nchi za visiwa vidogo, Amerika ya Kusini, na Asia magharibi kupitia uwekezaji katika nishati jadidu (salama na safi) ili kupunguza uzalishaji wa gesi chafu, kuzalisha ajira, na kuimarisha uchumi wa ndani.

7 Kuwa na miradi ya nishati mbadala, salama na safi ambayo inapunguza mzigo wa kazi ya utunzaji jamii bila malipo, ambayo wanawake na wasichana hutumia hadi asilimia 75 ya muda wao wakiifanya.[7] (Programu za Kijinsia za nishati mbadala na safi zimethibitisha kuwa na manufaa mengi ya pamoja ya kiafya na ya kuongeza kipato)

## **Fedha za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi:** Wafeminia wa Kiafrika wanadai utoaji wa fedha za kutosha, zinazoweza kufikiwa kwa urahisi, zenye masharti nafuu, na zinazozingatia haki za binadamu na usawa wa kijinsia. Tunatoa wito wa kuongezeka kwa uwazi na uwajibikaji katika ahadi zinazotolewa na fedha zinazotolewa na nchi zilizoendelea. Tunadai

8 Kuundwa kwa kituo maalum cha utoaji fedha zisizo leta madeni kwa ajili ya hasara na uharibifu unaoletwa na mabadiliko ya tabianchi ili kusaidia kwa haraka nchi zinazoendelea kuathirika na zinazokabiliana na hasara na uharibifu unaosababishwa na majanga yanazohusiana na mabadiliko ya tabianchi. Si haki na ni kinyume cha misingi ya utu kwa nchi na jamii zinazoendelea kuachwa peke yao na kusukumwa kutumia rasilimali ambazo tayari ni chache au kuingizwa kwenye mzunguko usio na mwisho wa madeni kukabiana na majanga ambayo hawakuyasababisha.

9 Kutoa dola bilioni 100 za fedha za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa mwaka. Mahitaji ya fedha za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa nchi za Afrika yamekadiriwa kuwa dola bilioni 250 kila mwaka.[8] Kwa hivyo, **Lengo Jipya la Pamoja** kuhusu fedha za kukabiliana na tabianchi lazima litoe zaidi ya kiwango cha Dola za Kimarekani bilioni 100 huku likihakikisha hitaji la kuweka ongezeko la joto chini ya nyuzi joto 1.5.

10 Kuongeza fedha za miradi ya kuendana na mabadiliko ya tabianchi na kutoa pesa za ruzuku badala ya mikopo. Hii itaruhusu nchi zenye kipato cha chini ambazo tayari zina madeni makubwa na zinakabiliwa na mizigo ya madeni yasiyo endelevu kuwekeza kwenye mipango na miradi ya kuendana na mabadiliko ya tabianchi hasa ambayo hutoa msaada wa usalama wa kijamii na kuongeza uwezo wa jamii kukabiliana na majanga ya tabianchi, na pia kupunguza mzigo wa uhifadhi jamii hasa pale ambapo huduma za umma hazitoshelezi, zinafadhiliwa kidogo, au zinashindwa kutokana na athari mbaya za mabadiliko ya tabianchi.

---

7 https://www.globalcitizen.org/en/content/womens-unpaid-care-work-everything-to-know/
8 https://www.climatepolicyinitiative.org/publication/climate-finance-needs-of-african-countries/#:~:text=Africa's%20USD%202.5%20trillion%20of,12%25%20of%20the%20account%20needed.

11 Kutathmini upya utaratibu wa utoaji wa fedha kutoka kwenye taasisi na mifumo mbalimbali ili kuhakikisha utoaji wa fedha hizo unakuwa wa rahisi na unaendana na mazingira tofauti na mahitaji ya fedha ya makundi mahususi - hasa wanawake, vijana na wazawa. Hii ni pamoja na kufikiria upya njia ya kuelekeza fedha za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi zinazohitajika hasa katika kukabiliana na hasara na uharibifu uliosababishwa na majanga ya mabadiliko ya tabianchi, kwa kuzielekeza kwenye jamii zilizoathirika baadala ya miradi iliyoandaliwa na mataifa ya kigeni na sekta binafsi.

12 Ushirikishwaji ulio na maana na uhusishwaji wa wanawake, wasichana, na vijana katika uaandaji wa vigezo vya utoaji na ugawaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, ikiwa ni pamoja na miradi ya kuendana au kukuondoa mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na uhamishaji wa teknolojia, na kuongeza uwezo wa katika ngazi zote.

13 Serikali na taasisi zinazotoa fedha za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi zitoe fedha kwa ajili ya kuwezesha kazi za maafisa wanaosimamia ujumuishwaji wa masuala ya jinsia kwenye malengo ya kitaifa ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

14 Kuimarisha uwezo wa serikali wa kupanga bajeti inayozingatia jinsia kwa ajili ya mipango ya mabadiliko ya tabianchi.

## **Haki za Kilimo na Ardhi:** wafeminia wa Kiafrika wanadai

15 Kupanua wigo wa upatikanaji na umiliki wa ardhi, rasilimali zalishi, na ufadhili usio na madeni kwa wanawake,  kwa ajili ya kilimo cha kiikolojia na  upatikanaji wa uhakika na uhuru wa chakula.

16 Ulinzi wa haki za wanawake wakulima wadogo na wazalishaji wa chakula, wavuvi wa wadogo, wafugaji, na wazawa kutokana na hasara na uharibifu unaosababishwa na mabadiliko ya tabianchi, kufukuzwa kwenye shughuli zao, unyanyasaji na vurugu.

17 Kuheshimu haki za jamii hasa haki za wakulima wa jadi na kulinda kikamilifu kilimo na mifumo ya mbegu na chakula asilia, kama inavyosisitizwa katika Mkataba wa Kimataifa wa Rasilimali za Vinasaba vya Mimea kwa ajili ya Chakula na Kilimo.[9] (Juhudi hizi zitasaidia kuhudumia vyema afya za watu, ulimwengu, na chumi za jamii husika kwa kusaidia wazalishaji wadogo wa chakula, hasa wanawake. Uwekezaji katika mifumo endelevu ya chakula, inasaidia upatikanaji wa uhuru wa chakula na kusaidia nchi kupunguza utegemezi katika uzalishaji na uagizaji wa chakula kutoka nje unaoongozwa na mashirika ya ubepari mamboleo.)

9 https://www.fao.org/3/i0510e/i0510e.pdf

## **Teknolojia:** Wafeminia Waafrika wanadai

18 Kusitishwa mara moja kwa mazoezi ya "uharamia wa viumbe" (umiliki usioidhinishwa na unyonyaji wa kibiashara wa maarifa na rasilimali za vinasaba kutoka kwa jamii za wakulima na wazawa na watu binafsi au taasisi zinazotafuta udhibiti wa ukiritimba wa kipekee kupitia vibali rasmi vilivyotolewa kwa kutengeneza bidhaa (hataza) au hatimiliki ya bidhaa zinazotokana na uwezo wa kufikiri.) wazawa, na haswa wanawake kama walinzi wa rasilimali hizi, wamelinda na kuhifadhi rasilimali hizi kwa vizazi. Uharamia wa viumbe huzuia matumizi ya baadaye ya rasilimali hizi huku ukishindwa kufidia jamii ambazo rasilimali hizo zinatoka. Maendeleo ya kiteknolojia yanayohusiana na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yanapaswa kujumuisha na kufidia maarifa mahususi ya wazawa na wanawake, na kukidhi mahitaji yao mahususi - ikiwa ni pamoja na ufikiaji, matumizi-rafiki, uwezo wa kumudu, ufanisi, na uendelevu.

19 Kwamba uwekezaji wa sekta binafsi katika kuendana au kukabiliana na mabadaliko ya tabianchi usiwe mbadala wa uwekezaji wa umma. Msisitizo wa kupata faida hasa kwenye uwekezaji wa sekta binafsi humaanisha kuwa uwezo wa sekta binafsi kukidhi mahitaji mapana ya jamii wakati wa majanga yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi ni mdogo hivyo kuweka ustawi wa jamii hatarini. Ubinafsishaji mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi utakuza ubidhaishaji wa mbinu hizo, kuimarisha ukoloni mamboleo dhidi ya wale walioathirika kupita kiasi, na kukuza ubepari wa uliberali mamboleo.

20 Kuacha kufadhili fumbuzi danganyifu ambazo hazijafanyiwa majaribio, zisizo endelevu na teknolojia isiyofaa kutatua changamoto zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi ambazo zimethibitishwa kuwa si chochote zaidi ya miradi ya kuzalisha faida kwa ajili ya wawekezaji binafsi wa kigeni.

## **Kufunganisha na programu zingine:** Wafeminia wa Kiafrika wanadai

21 Ujumuishaji wa masuala ya jinsia katika sera za kitaifa, miradi, na bajeti zinazohusiana na mabadiliko ya tabianchi na upunguzaji wa hatari za maafa zinazosababishwa na unyanyasaji wa kijinsia na kuimarisha utoaji wa huduma na haki za kijinsia na afya ya uzazi. Mahususi zaidi, sekretarieti ya UNFCCC, maafisa wanaosimamia ujumuishwaji wa masuala ya jinsia kwenye malengo ya kitaifa ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi, mashirika na taasisi mbalimbali wanahimizwa kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi za serikali zinavyoshughulikia mabadiliko ya tabianchi, jinsia na huduma za afya, ili masuala ya huduma na afya ya uzazi yaweze kuunganishwa katika sera na miradi ya kukabiliana na tabianchi ngazi ya nchi, ikijumuisha Michango iliyoamuliwa Kitaifa (NDCs) na Mipango ya Kitaifa ya Kuendana na Mabadiliko ya tabianchi (NAPs).

22 Uandaaji wa mikakati ya kitaifa ya kujifunza inayoleta mabadiliko chanya ya kijinsia katika kukabiliana mabadiliko ya tabianchi ambayo pia inatambua umuhimu wa uongozi wa vijana na kuweka kipaumbele kwenye elimu ya uraia, ujuzi wa endelevu, stadi za maisha, taratibu za kisera, uanaharakati, na kuwashirikisha wasichana na wanawake kwa

njia iliyo na maana katika kutengeneza mikakati hii. (*Hatua kwa ajili ya Uwezeshaji wa tabianchi - ACE*)

23 Kuzingatia na kuimarisha usalama na ulinzi wa haki za binadamu, za wanawake na watetezi wa haki za mazingira, hasa katika maeneo yenye migogoro, kwa kupunguza kuenea kwa silaha za moto na kukemea matumizi ya nguvu za kijeshi.

24 Ulinzi wa vyanzo vya maji na mabonde ya maji kama vile misitu ya asili ili kuhakikisha usalama wa maji kwa jamii na faida itokanayo na kupunguza mzigo wa kazi kwa wanawake na wasichana. Haki ya binadamu ya kupata maji inapaswa kulindwa kupitia tathmini pana ya athari ya kimazingira na tathmini za kijamii kwa kutumia dira ya usawa wa kijinsia kabla ya miradi yoyote ya usimamizi wa maji inayovuka mipaka au kati ya nchi na nchi, ikiwemo miradi ya umeme unaozalishwa kwa kutumia nguvu za maji, kuidhinishwa.

25 Uhifadhi wa mifumo ya ikolojia ya bahari na ya pwani (kama vile delta za mito, milango ya mito, matuta ya mchanga, mikoko na miamba ya matumbawe) kwa kuandaa hatua madhubuti za kuendana, kukabiliana na kushughulikia athari mbaya za mabadiliko ya tabianchi na uchafuzi wa mazingira. Hii ni pamoja na kushughulikia kupanda kwa kina cha bahari, ongezeko la joto la bahari, na kuongezeka kwa tindikali baharini.

26 Mafungano thabiti na mifumo mingine ya sera za kimataifa, kama vile **malengo/ makusudio ya Mkataba wa Bioanuwai (CBD)**, **Mfumo wa Sendai wa Kupunguza Hatari za Maafa** na **Jukwaa la Usawa wa Kizazi la Hatua za Kifeministi kwa ajili ya tabianchi**. Kwa kuweka msisitizo katika mafunzo na ujengaji wa ubia na ushirikiano ili kuhakikisha kuwa harakati za upunguzaji wa hatari za maafa na jitahada za kuimarisha ustahimilivu jamii zinaoongozwa na jamii yenyewe, na vipaumbele vya jamii katika uhifadhi vinafadhiliwa na kutekelezwa kwa kiwango cha kuridhirisha.

27 Kuhama kutoka kwenye mifumo ya kiuchumi ya kibepari na uliberali mamboleo ambayo inanyonya kupita kiasi, bila haki, na kwa njia isiyo endelevu kwa maliasili, mazingira na utu wa wanawake ili kushibisha tamaa ya watu wachache na nchi chache kwa gharama ya maendeleo endelevu kwa nchi nyingi zinazoendelea na ustawi ulimwengu.

## KUHUSU KIKOSI KAZI

*Mnamo mwezi Januari 2022, kikundi kidogo cha wafeminia wa Kiafrika, wengi wao wakiwa washiriki wa muda mrefu wa jukwaa la jinsia na wanakawe walianzisha Kikosi Kazi cha wafeminia wa Kiafrika kwa ajili ya COP27 kwa lengo la kuhamasisha wanaharakati wa Kiafrika kabla ya mkutano wa COP27 utakaofanyika nchini Misri na kuhakikisha kwamba sauti, matakwa, matarajio, na maono ya watetezi wa haki za wanawake yatakuwa sehemu ya michakato na matokeo ya COP27. Mwezi Aprili 2022, wito ulitolewa kwa umma kujiunga na kikosi kazi ili kupanua uwakilishi na ushirikishwaji. Hadi sasa, zaidi wa wafeminia 150 ni sehemu ya kikosi kazi cha wafeminia wa Kiafrika. Uanachama wa kikosi kazi uko wazi kwa kila mtu anayejitambulisha kama mpigania haki za wanawake kutoka Afrika.*